GIRLS NOT BRIDES | The Global Partnership to End Child Marriage

# KUKABILIANA KWA UFANISI DHIDI YA UKEKETAJI/UKATAJI NA NDOA ZA UTOTONI

## UTAFITI WA MSICHANA EMPOWERMENT KURIA, KENYA

***Shirika mwanachama wa Girls Not Brides***: Msichana Empowerment Kuria (MEK)

**Nchi**: Kenya

**Tarehe ya kuanza na kuisha kwa mradi**: 2015 hadi sasa

**Inadhaminiwa na**: FRIDA The Young Feminist Fund, American Jewish World Service, Hivos

## Muhtasari

Utafiti huu unaangazia umuhimu wa mikakati ya kina ya kuzuia ndoa za utotoni na ukeketaji/ukataji wa wanawake (FGM / katika muktadha wa Kuria, nchini Kenya. Unachunguza ugumu wa kukabiliana na masuala haya, inaangazia mbinu zenye ufanisi na inashiriki maarifa muhimu yaliyotolewa na Msichana Empowerment Kuria (MEK). Mbinu zenye ufanisi ni pamoja na **kuwawezesha wasichana kubaki shuleni, kuwezesha upatikanaji wa haki, kuwaimarisha wasichana, kushirikisha jamii** na **kujenga ushirikiano mzuri**. Uingiliaji huu umewezeshwa na ushirikiano thabiti wa asasi za kijamii (CBO) zinazofanya kazi pamoja nchini dhidi ya ndoa za utotoni na ukeketaji.
Utafiti huu unapaswa kuhamasisha wengine na kuchangia mijadala na kujifunza miongoni mwa mashirika wanachama ya *Girls Not Brides*.

Pia inaonyesha umuhimu wa ufadhili wa muda mrefu kwa CBO na kuwezesha mabadiliko ya kijamii, kwani wanaelewa vizury vizuri zaidi muktadha wa mitaa na mahitaji ya wasichana wanaowahudumia. Imeidhinishwa chini ya.



RAMANI: Eneo la kaunti ya Migori, mkoa wa Magharibi nchini Kenya, Afrika Mashariki. Na NordNordWest, CC BY-SA 3.0 DE.

## Asili ya ukeketaji na ndoa za utotoni huko Kuria

Ukeketaji na ndoa za utotoni ni haramu nchini Kenya: Ukeketaji kwa mujibu wa Sheria ya Marufuku ya Ukeketaji wa Wanawake ya mwaka wa 2011 na ndoa za utotoni kwa mujibu ya Sheria ya Ndoa ya 2014, ambayo inaweka umri wa ndoa kuwa miaka 18 bila ubaguzi. Pamoja na hayo, asilimia 23% ya wasichana nchini Kenya wanaolewa kabla ya umri wa miaka 18, na 15% ya wasichana wenye umri wa miaka 20 hadi 24 tayari wamefanyiwa ukeketaji.[1] Walakini, kuna tofauti kubwa katika kuenea kwa desturi hizi nchini Kenya.

Jamii ya Wakuria ni kabila ndogo lilopo Kaunti ya Migori, Magharibi mwa Kenya. Katika mila ya Kikuria, ukeketaji[2] ni desturi ya mpito ambayo hutangulia ndoa, kwa kawaida hufanyika wakati msichana ana umri wa miaka 13 hadi 14, lakini hivi karibuni kwa umri wa hata miaka nane. Kwa sababu ukeketaji unaonekana kutangulia ndoa za utotoni, wasichana wengi ambao hufanyiwa ukeketeji huolewa mara tu baada ya kupona. Wakiwa na asilimia

## Viendeshi vya Ukeketaji na Ndoa za Ututotoni

### Kanuni mbaya za kijamii

- Ukeketaji hutangulia ndoa za utotoni.
- Ukeketaji hutumiwa kutuliza miungu na ina misingi ya kanuni hatari za kijinsia.
- Uchawi ni kikwazo kikali katika kijamii, kwani wazee hutishia kuwalaani watu wasiofuata maagizo yao.
- Ukeketaji huonekana kuchangia mtu kuwa "Mkuria halisi." Wale wanaokwenda kinyume nao huonekana kutishia desturi ya maisha ya jamii nzima.
- Wasichana ambao hawajafanyiwa ukeketaji wanakabiliwa na vikwazo vikali vya kijamii na kutengwa.
- Wasichana walio na kiwango cha chini cha elimu wana uwezekano mkubwa wa kufanyiwa ukeketaji/ndoa ya ndoa za utotoni.

### Kiuchumi

- Wazazi hupokea mahari (ng'ombe 10 hadi 15) wanapowaoza binti zao.
- Watahiri hupata KSh 1,000 (takriban US$9) kwa kila msichana wanayefanyia ukeketaji.
- Umasikini pia umeenea katika eneo hilo.

## Changamoto za Kuweka Mikakati

- Kihistoria, mikakati ya kukabiliana na ukeketaji hupuuza wasichana wadogo, na kusababisha wasichana kukeketwa wakiwa na umri wa miaka nane.
- Wafanyakazi wa miradi wanaweza kupata vitisho na kushtuka, na hilo huathiri ustawi wao wa kimwili na kiakili.
- Ufadhili wa mizunguko mifupi hufanya mabadiliko endelevu kuwa magumu kufikia.
- Kuna "vituo" vichache vya uokoaji, ambavyo pia ni vya muda tu.
- Mitazamo mibaya kuhusu wasichana ambao hawajakeketwa hufanya iwe vigumu kujenga uaminifu na heshima katika jamii.

---

[1] Shirika la Kitaifa la Takwimu la Kenya, *Utafiti wa Idadi ya Watu na Afya nchini Kenya 2014, 2015*

[2] WHO infafanua ukeketaji kama "desturi ya kitamaduni inayodhuru ambayo inahusisha kuondolewa kwa sehemu au kuondolewa kabisa kwa sehemu za uke au kujeruhi sehemu za uke kwa njia nyingine kwa sababu zisizo za kitiba."

ya 84%,[3] jamii ya Wakuria ni baadhi ya jamii zilizo na uenezi mkubwa zaidi wa ukeketaji nchini Kenya. Kaunti ya Migori pia ina idadi kubwa zaidi ya kati ya ndoa[4] za kwanza za umri wa chini zaidi nchini Kenya, huku wasichana na wanawake wakiolewa wakiwa na umri wa wastani wa miaka 17.1.[5]

Kama ilivyo katika mazingira mengi, ukeketaji huaminika kuhakikisha ubikira wa kabla ya ndoa na uaminifu kwenye ndoa – na hivyo kuongeza uwezakano wa kuoleka kwa wasichana – kwa sababu inapunguza raha na ashiki yao ya ngono. Walakini, ukeketaji pia unahusishwa na imani za kijadi za Wakuria, na hutumiwa katika uchawi na kutuliza miungu yao. Ukeketaji – na mila inayoizunguka – hufanywa kwa siri, ikiongozwa na wazee wa jamii. Wazee hawa ni washawishi wakuu na watoa maamuzi. Wanajulikana kuwa na uwezo wa kulaani wale wanaowapinga na kwa hivyo hawapati upinzani kutoka kwa wanajamii.

Kabla ya kutangaza kuanza msimu wa ukeketaji, wao hufanya mila ya kutuliza miungu na kujilinda dhidi ya kifo. Desturi za mpito – sherehe zinazotokea wakati wa ukeketaji – hufanyika katika maeneo yaliyo mbali na wanajamii wengine, na zinaweza kuendelea kwa siku kadhaa. Vifo hutokea, lakini idadi halisi haijulikani kwa sababu ya usiri wa mila na wazee kutokuwa tayari kupiga ripoti. Kufa wakati wa ukeketaji huonekana kama ishara mbaya, kwa hivyo miili ya wasichana hao hutupwa katika maeneo yaliyo mbali na ardhi za jamii na wazazi hukatazwa kabisa kushiriki msiba wao na wanajamii wenzao.

Baada ya ukeketaji, wasichana hupewa mwezi mmoja wa kupona, na kwa wakati huo wanahimizwa kufanya ngono na wavulana waliotahiriwa, na hili husababisha mimba zisizopangwa. Wazazi ambao wana uwezo huwasaidia wasichana wao kuavya mimba, lakini wale ambao hawawezi wanaweza kumpa binti yao mwanamke mzee ambaye hana uwezo wa kupata watoto. Atamtafutia msichana huyo mume, ambaye atatarajiwa kupata watoto wengi iwezekanavyo naye. Yeye na watoto wake watadhulumiwa na hawatarithi mali yoyote kutoka kwa mwanamke huyo wala familia yake. Kitendo hiki huitwa "Nyumba mboke."

Wasichana ambao hawajafanyiwa ukeketaji wanakabiliwa na vikwazo vya kijamii ambavyo huendeleza desturi hizo na hata kuwahimiza wasichana kufanyiwa ukeketaji wasipopata msaada kwa wakati unaofaa. Vikwazo hivi vinajumuisha kutoruhusiwa kuchota maji kwenye sehemu za kuchotea maji, kuvuna mashambani, kuongea au kucheza na wasichana waliokeketwa, na kushiriki katika sherehe za kijamii kama vile harusi, na vile vile kunyimwa matunzo na wazazi, unyanyasaji kupitia mazungumzo na uonevu.

## Mbinu za MEK

Msichana Empowerment Kuria (MEK) ni asasi ya kijamii inayoongozwa na wanawake vijana iliyopo Kuria Mashariki, Kaunti ya Migori, Kenya. Dhamira yao ni kuwawezesha wasichana kupitia mbinu na mipango inayowalenga watoto wa kike ili kukomesha

[3] Shirika la Kitaifa la Takwimu la Kenya
[4] Data zilizochanganuliwa kuhusu kuenea kwa ndoa za utotoni, yaani asilimia ya wasichana wanaoolewa kabla ya umri wa miaka 18, hazipatikani kuhusu jamii ya Wakuria au Kaunti ya Migori. Kiwango cha ndoa za utotoni nchini Kenya ni 23% na kiwango cha ukeketaji ni 21%.
[5] WHO, *Female genital mutilation*, n.d.

ukeketaji na ndoa za utotoni. "Msichana" ni neno la Kiswahili linalowawakilisha mtoto wa kike.

MEK wanaamini kuwa ili kukomesha ukeketaji na ndoa za utotoni, wasichana ambao hawajakeketwa wanahitaji kuwezeshwa kukataa, na kwamba wale ambao hawajapitia desturi hizo wanapaswa kuwa na uwezo wa kuchagua kutowapitisha watoto wao desturi hizo.

Hatimaye, MEK inatarajia kusaidia jamii kukomesha ukeketaji na ndoa za utotoni. Malengo yao ya muda mfupi ni kupunguza hatari ya wasichana wanaopitia desturi yoyote kupitia:

1. Kujenga wakala wa wasichana kupitia vikao vya stadi za maisha na vya uimarishaji.
2. Kuwezesha upatikanaji wa elimu, huduma za afya na haki.
3. Kutumia mazungumzo ya jamii kuongeza uelewa wa jamii kuhusu athari mbaya za ukeketaji na ndoa za utotoni.

Shughuli za mradi wa MEK hushughulikia nguzo tatu kati ya nne za kimkakati katika Nadharia ya Mabadiliko ya Girls Not Brides: kuwawezesha wasichana, kuongeza ufikiaji wa huduma, na kuhamasisha familia na jamii.



PICHA: Natalie Robi Tingo na wafanyakazi wenzake wa MEK katika kaunti ya Migori, Magharibi mwa Kenya. Picha: Natalie Robi Tingo.

## Washirika wa MEK

MEK hufanya kazi haswa na wasichana wanaokwenda shule wenye umri wa miaka minane hadi 14, hivyo basi kujaza pengo lililoachwa na mikakati ambayo haishughulikii ukeketaji wa wasichana wadogo. MEK pia hushirikiana na wazazi wa wasichana na wavulana.

Wanakubali kuwa ukeketaji na ndoa za utotoni – ziwe zimewekwa pamoja au kipekee – ni masuala magumu sana, hamna shirika linaloweza kuzikomesha bila usaidizi. Kwa hivyo wanategemea mtandao wa mashirika ya nchini yanayofanya kazi katika maeneo tofauti na/au kutoa hatua tofauti ili kuboresha juhudi zao na kuhakikisha kuwa mkakati wao ni madhubuti.

## Washirika Wakuu

- Mkakati wa Nyanza wa Elimu na Uimarishaji wa Wasichana (NIGEE) wanashirikiana na MEK kutoa mazingira salama kwa wasichana wakati wa msimu wa ukeketaji, na kuwapa udhamini wa masomo. Walifanya kazi pamoja wakati wa msimu uliopita wa ukeketaji na walifadhiliwa na Bodi ya Kupambana na Ukeketaji nchini Kenya, ili kuendesha "kituo" cha uokoaji.
- Mtandao wa Wanawake Wahamasishaji Wakuria wa GOCESO ni kikundi cha wanawake wakubwa ambao huwashauri wasichana waliokeketwa na ambao hawajakeketwa walioacha shule, na huwasaidia katika kupata ujuzi wa kiufundi katika upishi na ushonaji nguo. MEK hushirikiana na kikundi hiki ili kuwapa wasichana msaada wa kisheria, kwani GOCESO ina mtandao mzuri wa rufaa wa wanawake 52.
- Zinduka - Neno linalomaanisha "amka" au "tokea" – hushirikiana na MEK kutoa msaada wa kisaikolojia kwa wasichana waliokeketwa na ambao hawajakeketwa, na kusaidia vikundi vya kijamii kuanza shughuli za kukuza mapato kwa kuwapa mtaji wa kuanza na mafunzo.

## Shughuli za MEK

### 1. Kujenga wakala wa wasichana kupitia vikao vya stadi za maisha na vya uimarishaji.

**Programu za kukuza stadi za baada ya shule**. MEK inafanya kazi na shule kadhaa huko Kuria ili kutoa mpango wa kusimulia hadithi zenye misingi ya haki za watoto ili kukuza elimu na kujenga stadi za maisha, talanta na ujuzi wa haki. Mpango huu hutumia jumbe zilizoandaliwa kwa uangalifu kuhusu ukeketaji, ndoa za utotoni na afya na haki za kingono na uzazi (SRHR), na huwashirikisha washauri wachanga wazungumze na wasichana waliokeketwa na ambao hawajakeketwa. Takriban watoto 300 hushiriki kila wiki kupitia vilabu hivi.

MEK pia inatoa mpango wa mafunzo ya ujuzi wa mwaka mzima – "Naweza" au "I can" – kwa kuzingatia hasa ukeketaji kwa wasichana ambao wako karibu kuacha shule. Pia hutoa mafunzo ya uwezeshaji wa kiuchumi kwa wazazi wa wasichana.

### 2. Kuwezesha upatikanaji wa elimu, huduma za afya na haki.

**Kuwapa wasichana sare za shule.** Wasichana walio kwenye vilabu vinavyoendeshwa na MEK mara nyingi huonekana wamevaa sare za zamani, na baadhi ya wasichana wanaogopa kuziosha zisije zikararuka. Hii inaathiri kujistahi kwa wasichana na inaweza kuwasukuma kufanyiwa ukeketaji na kuolewa ili kuepuka aibu ya kwenda shuleni na sare hizo. MEK hutafuta fedha na kuwanunulia sare wasichana hawa, hivyo basi kuwahamasisha kukaa shuleni. Wameweka wasichana zaidi ya 1,000 shuleni kupitia mpango huu.

**Kuwezesha usafi wa hedhi.** Athari za umaskini kwa hedhi huwaathiri wasichana wote – na mahudhurio yao shuleni – katika kaunti yote ya Migori. Kwa wastani,

wasichana wa shule huko Migori hukosa kwenda shuleni kwa wiki moja kila mwezi kwa sababu ya hedhi na kukosa bidhaa za usafi. Kukosa kwenda shuleni mara kwa mara husababisha utendaji duni wa masomo, ambao unaweza kusababisha kuacha shule na kuongezeka kwa hatari ya ndoa za mapema. MEK inasaidia wasichana kukaa shuleni kwa kuwapa pedi za hedhi na habari kuhusu usimamizi wa usafi wa hedhi.

**Kutoa udhamini wa elimu** MEK kwa sasa inadhamini elimu ya wasichana watano ambao wameepuka ukeketaji ili wasome.

3. **Kuongeza mwamko wa jamii kuhusu athari mbaya za ukeketaji na ndoa za utotoni kupitia mazungumzo ya jamii**

**Utetezi unaoongozwa na jamii.** MEK inahusisha wazazi wa wasichana na wadau wengine muhimu – kama vile wavulana, wanaume na watu wazee – katika mazungumzo kuhusu ukeketaji na ndoa za utotoni, kwa nini inafanywa na athari zake mbaya. Hii pia inatoa fursa kwa mazungumzo kati ya vizazi, haswa wasichana bibi zao ambao wamepitia ukeketaji na wana mtazamo tofauti kuhusu umuhimu wa mabadiliko. MEK wamefikia zaidi ya vijana 100 na wanawake 600 kupitia mazungumzo haya.

**Kuandaa hafla kubwa za kijamii.** Jamii pia huhamasishwa kupitia hafla kubwa za kukuza uelewa- ikijumuisha maandamano ya kila mwaka na mikusanyiko ya kusherehekea Mabingwa wa Jamii wa EndFGM. Mabingwa huteuliwa na vijiji vyao kwa kuchukua msimamo dhidi ya ukeketaji.

## MAFANIKIO YA MEK

- **Kuongezeka kwa mwamko kuhusu ukeketaji na ndoa za utotoni.** Kuendelea kushiriki kwa hiari katika mazungumzo ya jamii, hafla, na mipango ya baada ya shule ni ushahidi wa kuongezeka kwa hamu ya kukomesha ukeketaji na ndoa za utotoni katika jamii.
- **Watu zaidi wa kuiga ambao wamkekuwa na maisha tofauti na ni mabingwa wa jamii katika kukomesha ukeketaji na ndoa za utotoni.** Wasichana ambao walikuwa kwenye programu kisha wakamaliza masomo yao ya chuo kikuu na hawakukeketwa wanarudi kuwashauri wengine kama watu wa kuiga. Wao ni thibitisho kwamba ukeketaji na ndoa za utotoni hazina manufaa ya kiafya au nyingine yoyote. Kadiri idadi ya watu wa kuiga wanaojulikana inavyoongezeka katika jamii, ndivyo mwamko na shinikizo la kijamii kukomesha ukeketaji linavyoongezeka.

### Kwa Takwimu

- **Kufikia 100%** ya wasichana kwenda darasa linalofuata.
- **Wasichana 83** walimaliza shule ya msingi bila kufanyiwa ukeketaji.
- **Wasichana 300** waliepuka ukeketaji wakati wa msimu wa ukeketaji kwa kujificha katika "kituo cha uokoaji" cha muda kilichotolewa kwa ushirikiano na NIGEE.
- **Kumekuwa na upungufu wa 30%** wa **wasichana** wanaofanyiwa ukeketaji katika vijiji ambapo MEK hufanya kazi ikilinganishwa na miaka 5 iliyopita.

- **Kuongezeka kwa uaminifu na kutambulika.** Mtandao wa mashirika yanayoshughulikia ukeketaji na ndoa za utotoni umepata uaminifu na kujulikana miaka inavyozidi kupita. Wazazi zaidi wanaheshimu mipango yao, na idadi inayoongezeka huwasindikiza wasichana wao kwenda kwenye "vituo vya uokoaji" na kuwatia moyo wajiunge na mipango ya shuleni. Mamlaka za mitaa, mahakama na polisi wanawatambua na wanawajumuisha katika mikutano muhimu.
- **Ushirikiano thabiti na kutengeneza mitandao katika masuala ya ukeketaji na ndoa za utotoni**, na mengine husika kama vile elimu na usafi wa hedhi. "Vituo vya uokoaji" vinavyoendeshwa katika misimu ya ukeketaji huonyesha nguvu ya ushirikiano huu na jukumu la mashirika tofauti katika visa kama hivi: shule za mabweni hutoa ufadhili wa vituo, na polisi na mamlaka ya mitaa hutoa ulinzi, kama vile kwa kuwapokea wasichana ambao wanatoroka, vituo vinaweza kushambuliwa na wanajamii.

## Changamoto ambazo MEK imekumbana nazo

- **Upinzani na vitisho kutoka kwa jamii huwafadhaisha wafanyakazi.** Wafanyakazi wa MEK wamekabiliwa na vitisho vikali kwa maisha yao ambayyo vimewalazimisha kuondoka kwenye jamii kwa muda kwa ajili ya usalama wao. Wafanyakazi, washauri, wasichana na wanajamii ambao wanapinga ukeketaji na ndoa za utotoni pia hutengwa na kukataliwa. Matukio haya ni ya kutisha na yanaweza kusababisha uchovu na unyogovu.
- **Kiwewe na uchovu kutokana na kuwa kwenye mstari wa kwanza wa kuchukua hatua wakati wowote masuala yanapoibuka.** Jukumu la wafanyakazi wa MEK linajumuisha juhudi nyingi za kihemko, ikijumuisha kushuhudia dhuluma na hata kifo. MEK imeanzisha kifurushi cha huduma ya kutunza ustawi wa kihemko kwa watu wanaofanya kazi hii ili kuwasaidia kuepuka mafadhaiko na kukabiliana na changamoto wanazopata.
- **Ufadhili wa muda mfupi hufanya iwe vigumu kuweka mikakati na kufikia mabadiliko endelevu.** Ukeketaji na ndoa za utotoni huendelezwa na kanuni zilizojikita kwenye jamii na uwekezaji wa muda mrefu na uvumilivu unahitajika. Licha ya hayo, mizunguko ya ufadhili kwa kawaida huwa ya mwaka mmoja tu, na hautoshi kuleta mabadiliko endelevu. Mashirika ya kimataifa ambayo yaliunga mkono MEK hapo awali na mashirika mengine ya nchini wameondoka kwenye eneo hilo kwa sababu ya viwango vidogo vya mabadiliko.

> ***"Kutengwa na jamii kwa sababu ya msimamo wangu dhidi ya ukeketaji ndiko kunanisikitisha. Sikaribishwi kwenye hafla zozote na hawanitembelei. Watoto wangu hawachezi na watoto wa majirani wengine. Hakuna mtu aliyehudhuria hafla ya kuchangisha karo ya binti yangu. Jambo hilo linasikitisha."***
>
> *Joseph, mwanajamii ambaye alikataa binti zake wafanyiwe ukeketaji*

- **Idadi ndogo na kutodumu kwa "vituo vya uokoaji" inafanya iwe vigumu kutoa msaada kwa wasichana wote ambao wanauhitaji.** Wasichana wote ambao hawajakeketwa huwa hatarini katika msimu wa ukeketaji, bila kujalisha umri au kabila lao. Wanawake kutoka jamii ambazo hazifanyi ukeketaji pia wako hatarini katika wakati huu, kwani wanaweza kutekwa nyara na kulazimishwa kufanyiwa ukeketaji. Vijana mara nyingi hufanya doria kwenye jamii zao, na baadhi ya wasichana hufanyiwa ukeketaji nje ya msimu kwa wakati ambapo hauchunguzwi sana, kuna utekelezaji mdogo wa sheria dhidi ya ukeketaji na "vituo vya uokoaji" huwa vimefungwa.
- **Mtazamo wa jamii kuhusu wasichana waliokeketwa ambao wanashiriki katika mipango inaweza kusababisha mipango kuacha kuaminika.** Katika "vituo vya uokoaji," wasichana hushiriki katika mafunzo na hupewa vyeti baada ya kumaliza. Kama njia ya kupinga, baadhi ya wasichana waliwekwa hadharani katika jamii – wakionyesha vyeti vyao – ili kukejeli "vituo vya uokoaji."

## Vidokezo sita muhimu ambavyo vimewezesha mpango wa MEK kufanikiwa

1. **Kazi ya kushughulikia ukeketaji na ndoa za utotoni inapaswa kutegemea uelewa wa visababishi vyao vya msingi.** Ukeketaji na ndoa za utotoni mara nyingi husababishwa na kanuni sawa za kijamii zinazodhuru, ikijumuisha ubaguzi wa kijinsia na nia ya kudhibiti ujinsia wa wasichana. Zote mbili zinaweza kushughulikiwa kwa njia sawa, kama vile mazungumzo ya kijamii kuhusu haki za wasichana. Walakini, ni muhimu pia kuelewa viendeshi tofauti vya desturi hizi – na maana za kijamii na kitamaduni zinazohusiana nazo – ili kupanga mawasiliano madhubuti ya kukuza mabadiliko ya mwenendo huu.
2. **Kujenga wakala wa wasichana na maarifa ya afya na haki za kijinsia na uzazi (SRHR) kupitia stadi za maisha na mipango ya uwezeshaji, kusaidia wasichana kukaa shuleni, na kushirikisha wazazi na jamii ni mikakati madhubuti ya kupunguza ukeketaji na ndoa za utotoni.** Inapotumiwa kwa pamoja huunda njia madhubuti ya kushughulikia mahitaji ya wasichana na jamii.
3. **Jamii zinapaswa kushiriki katika kutafuta masuluhisho endelevu ya mitaani.** Ilhali tunaweza kuiga njia zinazotumiwa kwingineko kushughulikia masuala kama haya, ujifunzaji unahitaji kuendeshwa na jamii ili kupata msaada wao. MEK iligundua kuwa, ingawa njia mbadala za mpito zimesaidia kupunguza ukeketaji na ndoa za utotoni katika mazingira mengine, hazijakuwa na ufanisi sana huko Kuria kwa sababu hazikubadilishwa zifae na kumilikiwa na jamii. Ufanisi katika jamii moja haimaanishi ufanisi katika nyingine, kwa hivyo kutumia njia moja kote kunafaa kuepukwa. Walikuwa na mafanikio makubwa walipotumia washauri wa eneo, watu wa kuigwa na washauri kutoka kwa jamii ya Wakuria ili kuboresha ushiriki. Watu hao tayari wana ushawishi ndani ya jamii; wanajulikana, wanazungumza lugha ya asili, wanaelewa utamaduni wao na changamoto za eneo hilo, pamoja na maneno ya mwiko na lugha inayokubalika.
4. **Kuunganisha juhudi dhidi ya ukeketaji na ndoa za utotoni, na kuziwasilisha kuwa masuala yanayohusiana ya huduma za afya na haki za kingono na uzazi kunaweza kusaidia kuongeza ufadhili wa miradi inayonuia kuzishughulikia.**

Kama ukeketaji hutangulia ndoa za utotoni takriban kila mara huko Kuria, zinahitaji kushughulikiwa kama masuala yanayoingiliana. Kwa kuwasilisha desturi hizi za kijinsia zenye madhara kama masuala ya SRHR, MEK na washirika wao wamechangisha fedha kutoka kwa wafadhili wanaounga mkono SRHR lakini hawajishughulishi na ukeketaji au ndoa za utotoni zikiwa peke yao.

5. **Ushirikiano wa kimkakati unaweza kuongeza msaada unaotolewa kwa wasichana.** Kwa kuwa mipango yao yanahusiana na shule, MEK wameshirikiana na mashirika mengine – shule, mamlaka za mitaa na CBO zingine – ili kuwapa wasichana makao salama katika msimu wa ukeketaji. Ushirikiano pia umewasaidia kuchangisha fedha - kwa mfano, kutoka Bodi ya Kupambana na Ukeketaji, Kenya - ili kuendesha "kituo cha uokoaji" pamoja na NIGEE. Wadau wa kupanga ramani kabla ya kuanza mradi wanaweza kusaidia kuelewa ni mashirika yapi yako katika nafasi bora zaidi ya kushirikiana na wadau tofauti. Katika kupanga ramani ya mienendo ya nguvu na wadau muhimu, MEK iligundua kuwa wasichana wanaoenda shule wenye umri wa miaka minane hadi 14, wazazi wao na wavulana kuwa vikundi ambavyo wanaweza kushirikiana nao zaidi. Wakiwa wanawake vijana pekee, waligundua kuwa hawakuwa na fursa nzuri ya kushirikiana na viongozi wa jadi, na kwa hivyo walishirikiana na GOCESO ambao walikuwa na uwezo mkubwa wa kufikia kundi hilo. Uelewa huu umesaidia MEK kuzingatia mipango yao na kukuza wakala wa wasichana.

6. **Mipango ya shule inapaswa kujumuisha wasichana waliofanyiwa na ambao hawajafanyiwa ukeketaji.** Kwa sababu ya kuwepo kwa unyanyapaa, vikwazo na hatari zinazoendelea kwa wale ambao hawajafanyiwa ukeketaji, ni muhimu kusaidia wasichana wote katika kuelewa wanayopitia na kupinga shinikizo la kufuata mkondo huo.

## Kuangalia mbele

Iwapo fedha zitapatikana, MEK inanuia kujenga makao ambayo yatatumika kwa mwaka mzima ili kuepuka wasichana kukeketwa nje ya msimu wa kitamaduni. Unaweza kuwasaidia kupitia ukurasa wao wa ufadhili wa omprakash.

Utafiti huu umefanywa kutokana na mahojiano na MEK na wafanyakazi wa washirika wao, na mazungumzo na wanajamii na tungependa kuwashukuru kwa muda wao na michango yao. Mahojiano yalifanywa na mshauri huru Liza Akinyi.